Tanzania Natural Resource Forum
Mtandao wa Maliasili Tanzania

Address: P.O. Box 15605, Olorien, Arusha, Tanzania.
Phone: +255 755 022267
Email: info@tnrf.org
Website: http://www.tnrf.org

Taarifa ya Mwaka ya Mweka Hazina wa TNRF.

Imewasilishwa Ijumaa tarehe 9/02/2007

Katika mkutano wa kwanza wa mwaka wa TNRF kwenye hoteli *77* Arusha.

UTANGULIZI
Wanachama, Mabibi na Mabwana.
Inanipa faraja kubwa kusimama mbele yenu na kuwasilisha ripoti ya fedha kwa mwaka 2006. Nitasoma kwa ufupi, kwa umakini na ufanisi wa hali ya juu.

MAPATO
Kwa kipindi chote hali ya fedha imeimarika kwa kiwango cha kuridhisha, kwa sababu tumeweza kupata fedha kutoka nyanzo tofauti na kwa wafadhili mbalimbali. Akaunti ya TNRF imepitiwa na maodita na wameandika taarifa mzuri.

Mapato yetu yameongezeka kutoka **Tshs 83,400,000** mwaka 2005 mpaka kufikia **Tshs 217,672,818** kwa mwaka 2006-2007. Vilevile kulikuwa na nyongeza ya **Tshs 11,829,671** kama mapato mengine (ya ziada).

Kama ilivyokuwa kwa miaka iliyopita,tunaendelea kupata ufadhili wa pesa kutoka mfuko wa mazingira wa Bradley (Bradley Fund for the Environment) na msaada wa watu wa Norway (Norwegian's People's Aid). Kwa nyongeza ni kwamba tuliweza kupata wafadhili wengine watatu ambao ni Ford Foundation, Sigrid Rausing Trust na Wilson Fund (wa jamii ya hifadhi ya wanyamapori kutoka New York).

Jedwali lifuatalo linatoa picha halisi ya ufadhili pamoja na kiwango cha pesa (kwa mwaka 2006)

	2006	
MFADHILI	**US$**	**TShs**
Norwegian Peoples Aid	-	30,000,000
Bradley Fund for the Environment	49,794	61,151,878
Wildlife Conservation Society	18,810	23,700,600
The Ford Foundation	46,468	58,549,680
The Sigrid Rausing Trust	27,535	36,346,992
Sand County Foundation	-	3,999,528
Wizara ya Maliasili na Utalii Tanzania	3,087	3,924,140
JUMLA KUU		217,672,818

MATUMIZI

Kwa haraka haraka nitawasomeeni kasma zilizotumika pamoja na kiwango cha matumizi katika kila kasma husika kwa mwaka 2006.
Matumizi kwa mwaka 2006, yalikuwa kama ifuatavyo:-

- TShs 53,508,340 kwa matumizi ya gharama za rasilimali watu (sawasawa na asilimia 34 ya bajeti)
- TShs 12,456,022 kwa matumizi ya shughuli za utawala (sawasawa na asilimia 8 ya bajeti)
- TShs 9,391,127 kwa matumizi ya kamati ya uongozi, shughuli za mtandao pamoja na kusaidia wanachama (sawasawa na asilimia 6 ya bajeti)
- TShs 67,046,051 kwa ajili ya shughuli zinazohusu utetezi pamoja na mikutano ya elimu (sawasawa na asilimia 43 ya bajeti)

MAELEZO	KIASI CHA PESA	ASILIMIA
Utetezi na mikutano ya elimu	67,046,051	43%
Rasilimali watu	53,508,340	34%
Utawala	12,456,022	8%
Kamati ya uongozi, mtandao na kuwasaidia Wanachama.	9,591,127	6%
Usafiri	5,450,283	3%
Mawasiliano na Uchapishaji	4,880,729	3%
Gharama za mtaji	3,329,748	2%
Gharama (za muda mfupi) za Rasilimali watu	973,800	1%
Total	**157,236,100**	

MIZANIA

Kwa ujumla hali ya sasa ya pesa kwa shirika la TNRF siyo mbaya. Wafadhili wetu wapya wameanza kutoa pesa katika kipindi cha kwota ya tatu na ya nne ya mwaka uliopita hivyo basi hii inamaanisha ya kwamba TNRF kwa sasa ina kiasi cha kutosha cha pesa kwa huu mwaka 2007. Hivyo basi TNRF itajitanua zaidi katika programu zake za kazi ili kuweza kukidhi mahitaji ya wadau na washirika wake. Kwa maana hiyo pesa kutoka katika mfuko wa Ford (Ford Foundation) kwa ajili ya mitandao ya jamii itachukua sehemu kubwa ya matumizi kwa kipindi kinachokuja.

MATARAJIO YA MATUMIZI

Ni matarajio yetu kwamba wafadhili wetu wataendelea kutusaidia na kutuunga mkono. Ingawa tunahitajika kwa kiasi kikubwa kuweza kufanya juhudi kuongeza kiwango cha kupata pesa ili kuweza kwenda sambamba na mikakati yetu mipya na kuweka mkazo zaidi katika mawasiliano na ushiriki wa wanachama. Lazima tuendelee kuhakikisha ya kwamba tunapata pesa kutoka kwa wafadhili mbalimbali kwa shughuli muhimu za sekretarieti kwa sababu kiasi cha pesa katika kipengele hiki ni kidogo na kuna hatari kubwa ambayo ipo inayoandamana na jambo hili.

Kwa nyongeza, tutatafuta pesa kwa kipindi kinachokuja ili kuweza kuboresha uwezo wetu wa mawasiliano na tutatafuta uungwaji mkono zaidi kutoka kwa wanachama wa makundi ya kazi kama vile makundi yanayohusika na kamati simamizi za mbuga za wanyama pamoja na ustawi wa maisha ya jamii pamoja na makundi ya hifadhi ya misitu ili kuweza kuboresha umadhubuti na ufanisi wao.

Mwisho, TNRF itaboresha mkakati wake wa ufadhili pamoja na kuandaa mpango mkakati wa ufadhili ili kuweza kuwa na dhana endelevu katika masuala ya pesa, kuepusha hatari zitokanzo na masuala ya pesa na kuzidi kuboresha mahusiano mazuri yaliyopo na wafadhili.

UTAWALA WA PESA

Ningependa kutoa taarifa ya kwamba tumemaliza kuandaa softiwea mpya ya mfumo wa uhasibu ambao unakidhi viwango vya kimataifa. Ningependa kuwashukuru PINGOs kwa kutuazima mhasibu wao na kufumba macho pale mhasibu huyo alipokuwa anafanya shughuli za TNRF baadala ya kufanya shughuli za PINGOs.

KUENDELEA KWA SIFA YA UKAGUZI WA VITABU VYA MAHESABU. Wanachama, Mabibi na Mabwana.

Ingawa TNRF ilipata usajili wake mwaka jana, na ilikuwa inafanya kazi na kulelewa na WCST (Wildlife Conservation Society of Tanzania).

Kwa mantiki hiyo, ningependa kutoa taarifa ya sifa ya ukaguzi wa vitabu vya mahesabu iliyotunikiwa kuanzia mwaka 2005 TNRF na WCSt (Wildlife Conservation Society of Tanzania). Tutaendeleza mahusiano yetu ya karibu na WCST hususani katika kuwasaidia kutatua mambo yanayohusiana na ukaguzi wa vitabu vya fedha. Ninaamini kwamba mratibu anaendelea kufuatilia hili jambo na muda si mrefu litakuwa limapata ufumbuzi.

WAKAGUZI WA VITABU VYA FEDHA

Mwaka huu ni mwaka wa kwanza tangu tumepata usajili kama asasi isiyo ya serikali na huu ni mkutano wetu wa kwanza wa mwaka. Hivyo basi, mratibu wa mradi alichagua wakaguzi wa vitabu vya mahesabu kutokana na mapendekezo aliyoyapata kutoka kwa muhasibu. Kwa kawaida ni mkutano mkuu wa mwaka ambao unatakiwa kuwaidhinisha wakaguzi hao.

Wakaguzi wa mwaka 2006 walikuwa wanajulikana kama VA BUSSINESS Assurance SERVICES. Kwa ujumla nimeridhishwa sana na kazi ambayo imefanywa na wakaguzi hao na msaada wao mkubwa walioutoa kwa wajumbe wa sekretarieti na ningependa kutoa maoni yangu kwa wajumbe

wa mkutano mkuu ya kwamba ninaomba tuendelee kutumia na kufaidika na huduma zao mzuri.

Wanachama, Mabibi na Mabwana.
Kwa maneno hayo machache, ningeomba kuhitimisha taarifa yangu kwa wajumbe wa mkutano huu mkuu.

Ninashukuru kwa kunisikiliza n**a ninasema Aksanteni sana.**